**HOTUBA YA MKUU WA MKOA WA SHINYANGA MHE. ZAINAB R. TELACK KATIKA UZINDUZI WA SEMINA YA VIONGOZI NA WATENDAJI WA MKOA NA WILAYA KUHUSU USAJILI WA VIZAZI KWA WATOTO WA UMRI CHINI YA MIAKA MITANO ILIYOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA OFISI YA MKUU WA MKOA YA SHINYANGA TAREHE 27 FEBRUARI, 2017**

*Afisa Mtendaji Mkuu wa RITA, Bi Emmy Hudson*

*Katibu Tawala wa Mkoa,*

*Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya,*

*Wajumbe wa kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa,*

*Makatibu Tawala Wasaidizi,*

*Makatibu Tawala wa Wilaya,*

*Wakurugenzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa,*

*Wawakilishi kutoka Ofisi ya Rais – Tamisemi na Wizara ya Mambo ya katiba na Sheria.*

*Waganga Wakuu wa Wilaya,*

*Wawakilishi wa Wadau wa Maendeleo – Unicef na VSO,*

*Wageni waalikwa wote,*

*Waandishi wa Habari,*

*Mabibi na Mabwana.*

*Habari za Asubuhi!!!*

*Ndugu Washiriki,*

Awali ya yote napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema, kwa kutuwezesha sisi sote kukutana mahali hapa tukiwa na afya njema kwa ajili ya semina yenye lengo la kutoa elimu kwa viongozi na watendaji kuhusu Mkakati wa Usajili wa Vizazi kwa Watoto walio na Umri Chini ya Miaka Mitano. Nachukua nafasi hii pia kuwakaribisha washiriki wote ambao ni wageni hapa Mkoani, niwahakikishie tu kwamba Shinyanga ni salama na shughuli zote zinafanyika kama zilivyopangwa.

Nakushukuru sana Kaimu Afisa Mtendaji Mkuu, Msajili Mkuu wa Vizazi na Vifo na viongozi wenzako kwa kunialika kufungua semina hii ambayo ni muhimu na inaweka msingi wa utekelezaji wa mpango wa usajili wa watoto.

*Ndugu Washiriki,*

Kwa namna ya pekee naipongeza Menejimenti na watumishi wote wa RITA kwa jitihada mbalimbali ambazo mmekuwa mkizifanya katika kutimiza malengo ya msingi ya uanzishwaji wa Wakala (Agency) ikiwa ni pamoja na kuboresha huduma za usajili na utunzaji wa kumbukumbu nchini zikiwemo za Vizazi. Nafikiri wengi tunakumbuka miaka ya nyuma jinsi ilivyokuwa changamoto kupata cheti cha kuzaliwa lakini sasa hivi wote ni mashahidi kwa maboresho yaliyofanyika.

*Ndugu Washiriki,*

Sote tunafahamu kuwa maisha ya mwanadamu yeyote yanaanzia pale anapozaliwa. Tukio la uzazi, maana yake ni ongezeko la idadi ya watu katika jamii na katika Taifa.

Kwa upande wa Serikali tukio hilo maana yake ni kuongezeka wajibu wa kutoa huduma mbalimbali kwa wananchi wake. Sababu hiyo inapelekea usajili, upatikanaji na utunzaji wa kumbukumbu sahihi za kila tukio jipya la kizazi kuwa jambo la msingi sana.

***Ndugu Washiriki,***

Takwimu za Vizazi ni kichocheo cha maendeleo nchini kwani Serikali huhitaji takwimu hizi kwa ajili ya kupanga mipango ya maendeleo ya muda mfupi na muda mrefu. Ikumbukwe kwamba mipango mingi ya serikali huanzia katika ngazi za Mamlaka za Serikali za Mitaa, hivyo basi bila takwimu hizi ni vigumu kwa Halmashauri kuweza kujua kwa usahihi mahitaji ya kupeleka huduma muhimu kwenye jamii. Kwa mfano ni muhimu kujua katika miaka mitano ijayo kutakuwa na wanafunzi wangapi wanaohitaji kuanza elimu ya msingi, vituo vya afya vingapi vinahitajika katika eneo husika, nk. Afisa mtendaji mkuu wa RITA katika hotuba yake ametoa mifano miwili dhahiri inayohusu changamoto tulizonazo katika shule zetu hapa shinyanga na sababu kubwa ya msingi ni kutokuwa na takwimu sahihi za wananchi tulionao.

***Ndugu Washiriki,***

Kama Afisa Mtendaji Mkuu wa RITA alivyoainisha Takwimu za Mkoa wa Shinyanga za watoto waliosajiliwa na kuwa na vyeti vya kuzaliwa kuwa ni **asilimia 9.4** tu, mimi kama Mkuu wa Mkoa nasema (na nimekuwa nikisema kwenye maeneo mbalimbali) kwamba Takwimu hizi

haziridhishi, ni lazima kuwe na mabadiliko hasa tukitumia fursa ya mpango huu uliobuniwa na Serikali ambao hivi karibuni utaanza kutekelezwa katika Mkoa wetu. Ni changamoto kubwa, lakini naamini inawezekana kukabiliana nayo na hasa pale ambapo wadau wote tutashirikiana kwa pamoja na kutimiza wajibu wetu kwa watoto.

***Ndugu Washiriki,***

Kwa mfumo uliopo, vyeti vya kuzaliwa vinapatikana katika Ofisi za Wakuu wa Wilaya tu. Tumesikia wote jinsi Mkakati huu utakavyotekelezwa katika Mkoa wetu, *tafsiri ya haraka ni kwamba kuanzia leo, vituo vya usajili na upatikanaji wa vyeti vya kuzaliwa kwa watoto wa umri wa chini ya Miaka Mitano kwa Mkoa wa shinyanga vitaongezaka kwani huduma hizo zitakuwa zikipatikana katika Ofisi za Watendaji wa kata na Vituo vya Tiba.*

Haya ni mageuzi makubwa na nichukue fursa hii tena kuwapongeza RITA kwa kuunga Mkono juhudi za Serikali za kugatua madaraka na kusogeza huduma karibu na wananchi kama ilivyo dhamira ya Serikali ya awamu ya tano.

***Ndugu Washiriki,***

Usajili ni muhimu sana kwa kila mwananchi kwani kila mmoja bila kujali umri hutumia cheti cha kuzaliwa kwa ajili ya kupata huduma nyingine za msingi. Naamini na ninaomba iwe hivyo kwamba RITA itabuni na kuleta mpango mwingine kwa ajili ya kundi la watu walio na umri zaidi ya miaka mitano kwani kundi hili nalo lina watu wengi na wengine ni wanafunzi ambao wanahitaji sana vyeti vyao vya kuzaliwa.

*Ndugu Washiriki,*

Mtendaji Mkuu wa RITA ametushirikisha takwimu za mafanikio ya utekelezaji wa mpango huu katika Mikoa ya Iringa na Njombe na tumesikia kwamba mafanikio hayo yamechangiwa na usimamizi thabiti uliofanywa na viongozi, hivyo basi Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya, Mganga Mkuu wa Mkoa, Wakurugenzi wa Halmashauri na wengine wote kuanzia sasa tujipange ili Mkoa wetu uingie katika Mikoa yenye mafanikio katika utekelezaji wa mpango wa usajili wa watoto.

***Naagiza kwamba, kila mmoja kwa nafasi yake akasimamie na kuratibu zoezi hili la Serikali kwa nguvu zote na pasiwepo mtu wa kuwakwamisha.***

*Ndugu Washiriki,*

Leo tuko hapa kupata elimu ya kina kuhusu masuala ya usajili. Nawaomba wote tufatilie mada zitakazotolewa kwa makini na tusisite kuuliza au kuomba ufafanuzi pale tunapokuwa hatujaelewa. Naomba kuwakumbusha kwamba cheti cha kuzaliwa hakitolewi kwa kila mtu isipokuwa tu kwa wale waliozaliwa katika ardhi ya Tanzania.

Mkoa wetu ni moja ya Mikoa ulio na muingiliano mkubwa wa wananchi wa nchi jirani kama vile Rwanda, Burundi, DR Congo, n.k. Hivyo, tunahitaji kusimamia kikamilifu kuhakikisha wanaopata cheti cha kuzaliwa ni wale wanaostahili tu na ndio maana leo tumewashirikisha wajumbe wa kamati ya ulinzi na usalama ya Mkoa ili tupate mawazo yao ya namna bora ya kuwadhibiti wasiostahili.

***Ndugu Washiriki,***

Ili kuweza kutekeleza mpango huu kwa mafanikio iko haja ya sisi kama mkoa kujiwekea malengo ya utekelezaji ambayo yatakuwa kama dira yetu, baada ya mafunzo na majadiliano katika semina hii naomba muweke maazimio ambayo binafsi nitafuatilia utekelezaji wake kwa karibu sana ili kujua ufanisi wake.

Napenda kuwakumbusha kwamba Serikali ya awamu ya tano inatumia kaulimbiu ya hapa kazi tu, katika mpango huu nataka kuona kauli mbiu hiyo ikitekelezwa kwa vitendo. Binafsi, sitamvumilia kiongozi au mtendaji yoyote atakayefanya kazi hii chini ya kiwango na kusababisha mkoa kutofikia malengo.

***Ndugu Washiriki,***

Afisa Mtendaji Mkuu pia ameeleza kuhusu Majaribio yatakayofanyika katika mkoa wetu kuhusu Mfumo wa TEHAMA. Nawaagiza wale wote watakaohusika katika zoezi hili wazingatie maelekezo ili kuweza kupata matokeo bora yatakayowezesha kupatikana kwa Mfumo bora wa Kutuma na kutunza kumbukumbu za waliosajiliwa. Mimi ni muumini wa matumizi ya teknolojia katika kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi. Hivyo, nitafuatilia pia kujua maendeleo ya majaribio hayo.

***Ndugu Washiriki,***

Narudia tena kwa kusema kuwa, naunga mkono Mpango huu na pale ambapo watendaji kutoka RITA mtahitaji msaada wowote ulio ndani ya

uwezo wa Mkoa naomba msisite kunishirikisha mimi binafsi au Katibu Tawala wa Mkoa.

***Naomba nikuahidi Kaimu Afisa Mtendaji Mkuu wa RITA kwamba, kama ilivyowezekana katika mikoa mingine na hapa Shinyanga itawezekana.***

***Ndugu Washiriki,***

***Baada ya kusema hayo, ninayo heshima sasa kutangaza kwamba semina hii kwa viongozi na watendaji wa Mkoa na Wilaya kuhusu usajili wa vizazi kwa watoto wa umri chini ya miaka mitano imefunguliwa Rasmi leo tarehe 27 Februari, 2017.***

***Ahsanteni sana kwa kunisikiliza***